

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:
Simu: 2203156/58
Fax: +25522203213
Tovuti: www.dsm.go.tz
Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA
3 Barabara ya Rashidi
Kawawa,
S.L.P 5429,
12880 -DAR ES SALAAM.
Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**RC MAKONDA KUSAIDIA WAGONJWA 1,000 KUPATIWA MATIBABU YA
MACHO NA MIWANI BURE**

Mwendelezo wa zoezi la **Upimaji wa Afya Bure** kwa wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam wenye Matatizo ya Macho linaendelea na sasa ni Huduma ya Matibabu ya Macho kwa Wananchi waliobainika kuwa na Matatizo ya Macho kwenye Kampeni ya RC Makonda ya Upimaji wa Afya Bure.

Zoezi hilo ni kufuatia ahadi iliyotolewa na Jumuiya ya Waislamu wa Dhehebu la Khoja Shia Ithnasheri Jamaat K.S.I.J iliyojitolea kumuunga Mkono RC Makonda kwa kujitolea Matibabu ya wagonjwa watakaobainika kuwa na matatizo ya Macho na Mtoto wa jicho kwenye Kampeni ya Upimaji Afya Bure iliyofanyika Mnazi mmoja

Zoezi hilo linasimamiwa na Madaktari bingwa wa Macho kutoka Hospital ya Muhimbili, Hindumandal na Ebrahim Haji.

Kutokana na uhitaji kuwa mkubwa Mhe. Makonda ameomba Taasisi hiyo kupima na kufanya matibabu kwa wagonjwa 1,000 badala ya 500 iliyoahidi ambapo wameridhia ombi hilo.

Amesema kuwa kwa kawaida Garama za upasuaji wa Macho ni kati ya Shilingi 900,000 hadi 1,000,000 pamoja na miwani hivyo kwa watu 1,000 ni sawa na Kiasi cha Shilingi Billioni Moja lakini kupitia wadau wagonjwa hao watapatiwa matibabu na Miwani **Bure** ili waone Matunda ya Serikali ya awamu ya Tano kupitia RC Makonda

RC Makonda anawahimiza wananchi wenye Matatizo ya Macho kufika kwenye kambi ya matibabu ya Macho iliyopo mtaa wa Hindragand Posta kila Jumamosi na Jumapili kwa kipindi cha Miezi Miwili ili wapatiwe Vipimo, Matibabu na Miwani Bure kwa wenye uhitaji.

Ameshukuru wadau hao kwa kumuunga mkono na kueleza kuwa lengo lake ni kuwawezesha wananchi wasioweza kumudu gharama za matibabu kupata huduma.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM

05/10/2017